



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Wednesday, 15th February, 2023
Third Assembly – Seventh Sitting

*[The County Assembly met at 10:15a.m. at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Hon. Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, welcome to our morning session. Yes, Clerk please?

MESSAGE

NOMINATIONS OF COUNTY CHIEF OFFICERS BY HIS EXCELLENCY, THE GOVERNOR,
HONOURABLE ABDULSWAMAD SHERIFF NASSIR

Good morning again Honourable Members. Honourable Members, I have a Message from His Excellency, The Governor with the letter reference MsaCG.APP/CECM/1/VOL.II/175 dated 3rd February, 2023, reference; Nomination of Chief Officers received by our offices on 13th February, 2023.

In accordance with the powers conferred upon me by the County Government Act, 2012 Section 45, I do hereby forward the following Nominees for vetting, approval and subsequent appointment as County Chief Officers as follows;

- | | |
|---|------------------------------------|
| 1. <i>Transport and Infrastructure</i> | <i>Eng. Albert Keno</i> |
| 2. <i>Lands, Housing & Urban Planning</i> | <i>Mr. Ali AbdulRahman</i> |
| 3. <i>Blue Economy, Agriculture & Livestock</i> | <i>Mr. Hamid Shehan Nanda</i> |
| 4. <i>Policy & Planning</i> | <i>Mr. Jibril Maalim Mohamed</i> |
| 5. <i>Environment & Solid Waste Management</i> | <i>Ms. Pauline Adhiambo Oginga</i> |
| 6. <i>Renewable & Energy, Natural Resources & Climate Change Resilience</i> | <i>Mr. John Kipyegon Kiprop</i> |
| 7. <i>Clinical Services</i> | <i>Dr. Shem Patta</i> |
| 8. <i>Education</i> | <i>Ms. Roselyn Sidi Randu</i> |
| 9. <i>Youth, Gender & Social Services</i> | <i>Mr. Khamis J. Kurichwa</i> |
| 10. <i>Digital Transformation</i> | <i>Mr. Anwar Said</i> |
| 11. <i>Public Service Administration</i> | <i>Mr. Justina Kavuu Mwikya</i> |
| 12. <i>Tourism, Culture & Trade</i> | <i>Mr. Swaleh R. Mwalizuma</i> |
| 13. <i>Finance & Economy Planning</i> | <i>Ms. Gloria Wandoe Mwasi</i> |
| 14. <i>Governance</i> | <i>Ms. Rukiya AbdulRahman</i> |

15. *Public Health & Disease Prevention*

Mr. Abdalla Daleno

16. *Water & Sanitation*

Ms. Marian Mapenzi

Please expedite the process.

Yours faithfully

H.E. Abdulswamad Sheriff Nassir

Honourable Members, Pursuant to Section 6(1) and Section 7(1b) of the Public Appointments, County Assembly Approval Acts, 2017, and Section 45(1b) of the County Government Act, 2012, these nominations stand committed to various Sectoral Committees for appropriate action. They include:

1. Eng. Albert Keno, Chief Officer Transport & Infrastructure stands committed to the Committee on Transport & Infrastructure;
2. Mr. Ali AbdulRahman, Chief Officer Lands, Housing & Urban Planning stands committed to the Committee on Lands, Housing & Urban Planning;
3. Mr. Hamid Shehan Nanda, Chief Officer Blue Economy, Agriculture & Livestock stands committed to the Committee on Blue Economy, Agriculture, Fisheries & Livestock;
4. Mr. Jibril Maalim Mohammed, Chief Officer Policy and Planning stands committed to the Committee on Justice and Legal Affairs;
5. Ms. Pauline Adhiambo Odinga, Chief Officer Environment and Solid Waste Management stands committed to the Committee on environment and solid waste Management;
6. Mr. John Kipyegon Kiprop, Chief Officer Renewable Energy Natural Resource and Climate Change Resilience stands committed to the Committee on Water and Natural Resource and Climate Change Resilience;
7. Mr. Shem Patta, Chief Officer Clinical Services stands committed to the Committee of Health;
8. Ms. Roseline Sidi Randu, Chief Officer Education stands committed to the Committed to the Committee on Education and Digital Transformation;
9. Mr. Khamisi Kurichwa, Chief Officer Youth, Gender and Social Services stands committed to the Committee Youth Sports Gender and Social Services;
10. Mr. Anwar Said, Chief Officer Digital Transformation stands Committed to the Committee on Education and Digital Transformation;
11. Mr. Justina Kavuu Mwikya, Chief Officer Public Service Administration stands committed to the Committee on Labor and Public Service;
12. Mr. Swaleh R. Mwalizuma, Chief Officer Tourism Culture and Trade stands committed to Committee on Tourism Culture and Trade;
13. Ms. Gloria Wandoe Mwasi, Chief Officer Finance and Economic Planning stands committed to the Committee on Finance, Budget and Appropriation;
14. Ms. Rukiya Abdulrahman, Chief Officer Governance stands committed to the Committee on Justice;
15. Mr. Abdalla Daleno, Chief Officer Public Health and Disease Prevention stands committed to Committee on Health;
16. Ms. Marian Mapenzi, Chief Officer Water and Sanitation stands committed to the Committee on Water Natural Resources and Climate Change Resilience;

Thank you. Yes Clerk, next order please.

PAPERREPORT ON THE REVIEW OF THE REVIEW OF THE TASKFORCE REPORT ON MOMBASA COUNTY
HEALTHCARE SYSTEM

Yes, Honourable Bernard Ogutu, please lay the Paper?

Hon. Ogutu: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker, I rise to lay the Report on review of the taskforce report on Mombasa Health Care System. Thank you.

[Paper Laid]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Chairperson Committee Health Services Bernard Ogutu for laying down the paper. Yes Clerk, next order please.

NOTICE OF MOTIONADOPTION OF REPORT ON THE REVIEW OF THE TASKFORCE REPORT ON MOMBASA COUNTY
HEALTHCARE SYSTEM

Yes, Honourable Bernard Ogutu, Chairperson Committee on Health Services please issue the Notice of Motion?

Hon. Ogutu: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to give Notice of the following Motion;

THAT, this House adopts the Report on Review of the Taskforce Report on Mombasa County Healthcare System laid on the Table on Wednesday, 15th February, 2023 during the 7th sitting.

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, the Motion by Honourable Bernard Ogutu, Chairperson Committee on Health Services will be moved on Wednesday 15th February, 2023 during the 8th sitting. Yes Clerk, next order please.

MOTIONESTABLISHMENT OF MASSIVE VOCATIONAL TRAINING AND UPSKILLING OF UNEMPLOYMENT YOUTH
AND WOMEN PROGRAMME

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Allen Katana, MCA Shanzu Ward please move the Motion.

Hon. Katana: Thank you Honourable Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion:

THAT AWARE THAT, the National and County unemployment rates are at all times high of 40 per cent for Mombasa County;

FURTHER AWARE THAT, many youths and women are affected by the ravaging unemployment phenomenon due to lack of adequate technical skills required in the competitive on market or lack skills to self-employment themselves;

COGNISANT THAT, the National government has similar programme for the youths but is limited in scope and scale;

NOTING THAT, youths and women are great human capital resource which if well harnessed and deployed could spur economic growth and county progress;

FURTHER NOTING THAT, the massive training programme should include life skills, ICT, cottage industries, entrepreneurship and other practical courses needed in the labour market;

CONCERNED THAT, if the ravaging unemployment and lack of technical skills is not seriously addressed at the County level, there risks sagging unemployment slow economic growth and attendant their ripple effects and continuation of other social malaise;

I, therefore urge this Assembly to RESOLVE:

THAT the County government of Mombasa to establish a massive training and up-skilling of technical skills programme for unemployed youths and women to address the skills gap and equip them for the competitive labour market and for self-employment.

Mr. Speaker, I humbly ask Honourable Mohamed Hamid to second the Motion.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Katana. Yes, Honourable Hamid?

Hon. Mohamed Hamid: I second the Motion.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Hamid. Honourable Members, I now propose a question that the Motion by Honourable Allen Katana MCA Shanzu Ward on establishment of massive vocational training and up-skilling of unemployed youth and women programme be considered by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Allen Katana, MCA Shanzu Ward please make your contributions.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa nafasi hii. Nitaongea kwa ufupi kwa sababu hili swala liko wazi na ni uhitaji wa mahali kwingi na limekuwa donda sugu kwa sababu watu hawajataka kujukumika Mheshimiwa Spika. Takwimu zinasema asilimia arubaini ya vijana na kina mama Kenya yote hii hawana kazi na tukija katika Kaunti yetu ya Mombasa asilimia hio hio tuko arubaini na nne sasa Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia sana utapata katika jamii hii yetu vijana na kina mama ni kikundi cha watu ambacho kwa hakika endapo watawezesha katika masomo fulani fulani kwa hakika itakuwa ni mtaji wa maana katika kuijenga na kuleta vipato katika Kaunti yetu hii.

Zaidi ya hayo Mheshimiwa, hii idadi ikiachiliwa iendelee kuongezeka kwa sababu kuna ukosefu wa kazi unaoletwa na watu kukosa ufahamu katika nyanja fulani fulani ambazo zinapatikana huku kwetu basi uhalifu utazidi na pia vilevile kama tujuavyo ndoa nyingi zinasimama sababu kuna kipato na ili kuzuia mambo mengi kama ukosefu wa usalama na ndoa nyingi kuvunjika kwa sababu ya ukosefu wa mapato ninacho amini ni kwamba endapo wapata mafunzo ili wajifundishe taaluma fulani ambazo zitawawezesha kupata ajira ndani na nje ya Kaunti yetu basi litakuwa jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, zaidi kama nilivyochangia kusema ya kwamba kina mama na vijana ndio ambao ni mtaji wa maana ambao endapo utapewa nafasi na ufanyiwe kazi basi kwa hakika tutakuwa tumewezesha familia nyingi na mbali na kupata kipato kikubwa katika serikali yetu ya Kaunti vilevile tutaweza kukimu mahitaji ya familia nyingi na hivyo basi kupunguza mambo mengi ambayo yanaweza kuwa ya madhara na kuharibu mazingara yetu mazuri ya kuishi katika jimbo letu la Kaunti hii. Mheshimiwa Spika, nimeonelea hili jambo likaweze kufana na likaweze kuleta manufaa ni vizuri watu wakaweze kufundishwa wapate masomo katika maisha yetu ya kawaida kama kazi za ndani wakawezeshwe maana huku kwetu pwani haswa jimbo letu hili la Mombasa vijana wengi hupata kazi za kuenda ughaibuni na wakifika kule viko vifaa vingine vinatumika kule na inakuwa kuwa hawa watu kwao kunapikwa na majiko ya mawe matatu wakienda kule inakuwa mitihani na inabidi warudi.

Kwa hivyo yale majukumu ya kawaida ya kinyumbani endapo watafundishwa Mheshimiwa Spika, watakapo enda kule bila shaka watakuwa wachapa kazi hivyo basi kupata kitu cha kuwezesha familia zao. Kama tujuavyo mji wetu wa Mombasa asilimia kubwa ni ya utalii; na endapo pia watu watafundishwa zile kazi zinazo husishwa na hizi nyumba za wageni kuja na kulala mbali na kwao kama kazi za kuwakaribisha wageni, kazi za kutandika vitanda vya wageni, kazi za kupika vyakula vya wageni na vitu kama vile itakuwa ni rahisi wao kujipatia kazi katika hizi tunazoziiita *cottages* na hizi hoteli pia za kifahari zilizo katika fukwe za bahari. Mheshimiwa Spika, masomo mengine ambayo ni muhimu watu wetu wakifundishwa hasa hasa vikundi hivi kina mama na vijana kama kufundishwa biashara, maswala na biashara kwa sababu kwa hakika itakuwa vigumu sana kuwaajiri vijana wetu na hawa wa mama. Sasa kwa kuwa ni vigumu kuwaajiri watu hawa wote ingekuwa ni vizuri wafundishwe jinsi ya kufanya biashara, alafu serikali hii yetu iangalie mbinu ambayo ikiwezekana hata wakaweze kupewa mtaji katika vikundi vyao na yale masomo watakayokuwa wamepata kwa sababu ya biashara ninataka kuamini Mheshimiwa Spika ya kwamba kwa hakika itawawezesha wao wenyewe na kujimudu katika maisha yao na tena nyanja nyengine ambayo inakuwa na karibuni dunia nzima watu wote wanaenda upande huo, ni maswala ya masomo ya kimtandao.

Mheshimiwa Spika ikiwa kufikia sasa hata hapa kuna Waheshimiwa ambao kidogo wako nyuma katika maswala ya kimitandao, utakuta kuna ugumu fulani kwa sababu dunia ya sasa karne hii tuliyofikia tuko katika mfumo wa dijitali. Kwa hivyo watu wetu, hawa vijana na akina mama endapo watakata mafunzo haya nina hakika kutatokea nafasi ambazo zitaweza kuwasaidia watu wetu na tutakapo fanya mambo haya mimi nataka kuamini Mheshimiwa Spika tutapunguza hili janga kubwa la ukosefu wa kazi. Kwa hayo nataka nikomee hapo Mheshimiwa Spika na ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Allen Katana for your contribution. Yes, Honourable Mwamwiri Majority Leader, please make your contribution.

The Majority Leader (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika awali mimpongeze Mheshimiwa wa Shanzu kwa hoja hii...

[Applause]

Kuzingatia umuhimu wa elimu na tajiriba katika soko la ajira. Mheshimiwa Spika ukosefu wa ajira ni nini? Ukosefu wa ajira Mheshimiwa Spika ni ile idadi ya watu ama watu ambao wapo maeneo lakini hawana kazi aidha kwa kustaafu ama kuachishwa ama wana vigezo au hawana vigezo wanatafuta kazi lakini hawajabahatika kupata kazi hiyo. Mheshimiwa Spika, janga hili ni janga la ki mataifa kwa sababu nchi zote duniani zina changamoto ya uwezo wa kuajiri vijana inavyo stahiki ili sisi kuwa mbele katika hili, ni kuandaa vijana wetu katika soko la ajira na kwa kuwezesha hilo ni lazima vijana wetu waweze kupata mafunzo kama mdhamini wa hoja hii alivyo pendekeza ya kwamba kama serikali tuweze kuwekeza kuhakikisha vijana wetu wanapitia masomo ama taaluma mbali mbali ambazo zinahitajika katika soko la ajira ili inapotokea fursa yoyote vijana wawe ni wa kwanza watapewa kipao mbele kabla kufikiriwa vijana wengine katika fursa hii.

Kwa mfano Mheshimiwa Spika, utakuta kanuni za ajira zinasema ya kwamba ajira yoyote inapotokea iwe asilimia sabini iwe ni wenyeji wa pale na baada ya hapo tutoke nje ya pale ikipanuka hadi iwe Kenya na kimataifa kwa jumla lakini Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufikia asilimia sabini swali ni; vijana wetu tumewaandaa kivipi ili kukidhia asilimia hii ya sabini kwa nafasi yoyote ikitokea lazima kama serikali tuweze kushirikiana na mdhamini wa hoja hii Mheshimiwa Allen tuweze kupitisha hoja hii na kuhakikisha tumewekeza inavyo stahiki vijana wetu tuwaandae na mafunzo haya kwa sababu gumzo kuu linalofuata sasa hivi ni *Special Economic Zone* ama uwekezaji wa viwanda na biashara katika eneo la Dongo Kundu. Mheshimiwa Spika, mulki wa wawekezaji watawekeza katika maeneo yale, kipao mbele ni vijana wetu wa ki Mombasa waweze kupata nafasi ya kwanza katika ajira zile, swali ni je, tumewaandaa vipi katika kulikabili lile?

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, niungane na nisihi Waheshimiwa wenza tuweze kumuunga mkono Mheshimiwa kupitisha hoja hii ili tuweze kuwa mbele ya mipango wakati viwanda vitakuwa vimeimarika na sisi vijana wetu wako tayari kupata ajira za hapa ndani lakini pia inapotokea ajira yoyote ya nje iwe tuna hakika ya kwamba kijana wetu anakwenda kule akiwa na ufahamu ni kipi atakapo enda fanya ilipia kuepuka haya maswala ya dhulma katika mazingira ya kikazi. Ahsante Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much again Honourable Majority Leader. Yes, Honourable Hassan Uheir please make your contribution.

Hon. Hassan Mohamed: Ahsante Bwana Spika kwa fursa ili kuweza kuchangia hoja ambayo imeletwa na kiongozi ambaye amefikiria kwa upana na ni jambo ambalo sisi kama viongozi katika kata tofauti tunakabiliana nalo ikiwemo sera zetu ambazo tuliwaahidi vijana, wananchi wa mama kwa ujumla kwamba tutaweza kukidhi mahitaji yao na mahitaji yao ni kuwapatia suluhu ya kudumu na suluhu ya kudumu ni ajira maana tayari wao washatuajiri. Kwa hivyo ni lazima kuregesha shukrani kwao, hivyo basi mimi naunga mkono asili mia moja hoja ambayo imeweza kuletwa na ndugu yangu na natumai kwamba Jumba hili lote litaweza kuunga ili nao wananchi wawe na imani na sisi. Ahsante sana Bwana Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Samuel Mwaura, please make your contribution.

Hon. Mwaura: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa niweze kuchangia katika suala hili napenda kuungana na wenzangu kuunga suala hili mkono kwa sababu ya kuwa juzi tulipokuwa tunaanza vikao nilileta Mswada wa kusema kwamba tuondoe vijana katika maeneo haya yetu ya Bunge na baadhi yetu tukazungumza tukasema hawa vijana wamekuwa hapa kwa sababu ya ukosefu wa ajira na hiyo ndio taswira ilioko maeneo yote, ya kwamba kuna vijana wengi katika mji huu wetu wa Mombasa ambao wanakaa na hawana mahali pa kutafuta riziki, wanakaa wengine wanaingililia mambo ya mihadarati, wengine wanaingililia mambo ya ukora hivi wakati huu tunavyozungumza hali ya usalama katika Mombasa yetu haiko sawa sawa na hii yote inasababishwa na vijana wetu kwamba hawajatayarisha kwa ajli ya kuingililia mipangilio ya ajira.

Mheshimiwa Spika kitu ambacho labda ningelipenda nielewe tu zaidi kama serikali yetu iko na utayari wa kuhakikisha kwamba haya mambo yamefanywa kwa sababu idadi ya vijana ambao wanahitaji mambo haya iko juu sana na ninaamini ya kwamba fedha zinazo hitajika kwa ajili ya jambo hili ni fedha nyingi so napenda kuiunga mkono na pia waweze kuangazia suala hilo la kupatikana kwa fedha kwa ajili ya mambo haya tusije tukawa kila siku tunapitisha jambo hapa linahitaji fedha halafu yale ambayo tunapitisha yanaendelea tu kukaa katika makabati na hayatekelezwi. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nasimama kuunga mkono jambo hili. Ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Samuel Mwaura. Yes, Honourable Salim Mbaya, please make your contribution.

Hon. Salim Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa kabla ya kusonga mbele nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia fursa hii na kuweza kukutana siku ya leo tena kuweza kuizungumzia jamii yetu ambayo imeweza kuona kwamba tunatosha tuwe viongozi wao. Mheshimiwa Spika kwanza kabisa mimi napenda nimpongeze Mheshimiwa Mwenza Allen Katana kwa jina la utani 1GB...

[Applause]

...Kwa kuja na fursa adimu ya kuweza kujali vijana wetu kwa sababu ujana ni moshi na ukipita haurudi na kwa hakika kabisa Mheshimiwa Spika kutokana na umri wetu mahali tumefikia kama sisi tukikumbuka wakati wa ujana ndio ulikuwa wakati rasmi wa maisha yetu kuringia tofauti na vile tunavyoringa saa hii. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika kuhusiana na vijana kuwakuza vipaji vyao ili waweze kupata ajira mimi naona hilo sioni kama kuna mwanadamu atakuwa na nafasi ya kupinga kwa sababu sisi sote tumepitia ujana na ujana ni moshi ukipita haurudi. Kwa hiyo mimi namuunga mkono Mheshimiwa Allen Katana 1GB kwa jina la utani kwa asilimia 90 kwa mia...

[Applause]

...ili vijana wetu waweze kupata mafunzo na waweze kupata ajira kwa sababu ujana ni moshi na ukipita haurudi. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Salim Mbaya. Yes Honourable Nusura Mwinyi please make your contribution.

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Kwanza nataka nimpongeze sana Bwana Allen Katana kwa kuileta Hoja hii ndani ya Bunge hili; kwa kusema kweli umefanya jambo la maana sana kwa sababu kwa maana hiyo tutapunguza maskani kwanza, tutapunguza ulaji wa Muguka, tutapunguza uvutaji bangi endapo Hoja hii tutaipitisha hapa ndani ya Bunge na masuala haya yatafuatilizwa vilivyo. Mimi nataka kusema kule mitaani vijana wako wengi sana, naona hapa imeandikwa asilimia 40 lakini naona labda ni zaidi kwa sababu maskani ni nyingi na vijana hawana ajira na kitu ambacho nitasema kinawafanya wakose ajira labda hawana ujuzi ama hawana pia stakabadhi kwa wakati huu mahali popote utakapokwenda labda kutafuta ajira kwanza utaulizwa labda stakabadhi ama umefanya ujuzi gani pengine ndio angalau upatiwe ajira. Kwa maana hiyo Hoja hii itatuletea nafasi nzuri ambayo tutapunguza ukora ama uhuni, nataka kusema kule kule mitaani wale wale vijana jamani ni wagumu sana pia kusema wanaenda kutafuta ujuzi kwa hivyo sisi kama viongozi ningependa tuanze na sisi tuwaite tuweze kuwaelimisha tuwaambie maisha ni nini, tuwaambie wako wapi na wanaelekea wapi ili pia nao wajifahamu kwa sababu ajira zitakuja na vijana wetu watakuwa hawana ujuzi ama hawana stakabadhi. Kwa hivyo nimesimama kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Nusura. Yes, Honourable Sylvester Kai please make your contribution.

Hon. Kai: Ahsante Mheshimiwa Spika kuweza kunipatia fursa hii niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Allen Katana. Kiukweli ni hoja mwafaka sana na imekuja kwa wakati mzuri ambao kwa kweli vijana kule nje wana mahitaji makubwa ya kazi, wanashinda kwa majumba zetu wakituulizia kazi lakini ukweli kabisa asilimia kubwa ambapo naweza kuipatia asimilia themanini kwa mia wengi hawana ujuzi wa aina yoyote hata ukimuuliza ni kazi gani anakwambia ni kazi yoyote. Mheshimiwa Spika, kwa hivyo matayarisho yoyote ya kuwawezesha angalau hawa vijana wakaweze kuwa na ujuzi maalum itakuwa inaweza kuleta mwafaka mkubwa. Lakini vilevile nikubaliane na dadangu Mheshimiwa Nusura ya kwamba hawako tayari kwa kiasi kikubwa ya kwamba waende shuleni wapate ujuzi wa aina yoyote kikubwa kinacho wafurahisha zaidi ni jambo ambalo litawapatia pesa leo na kama sio leo iwe ni kesho. Kwa hivyo kuna haja kubwa ya pia serikali yetu ya Kaunti ikaweze kufikiria ya kwamba sio hasara tukiweza kuanzisha program ambayo itawasaidia wakaweze kuhamasishwa kuelewa ya kwamba kesho yao lazima wakaweze kuitengeneza hivi leo na ni kwa kupitia kwao kurudi shuleni na kupata ujuzi sanasana taaluma ya mkono. Hivyo Mheshimiwa Spika nikaweze kuchukua fursa hii kuunga mkono na pia niulize Waheshimiwa wengine katika Jumba hili tukaweze kuweka vichwa vyetu pamoja na kuanza kuleta hoja katika Nyumba hii ambazo zitakuwa zinaleta natija ya kusaidia hawa ndugu zetu na mama zetu kule majumbani...

[Applause]

Niseme ahsante sana na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja chini ya mia moja. Shukran.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Sylvester Kai. Yes, Honourable Manuari please make your contribution.

Hon. Juma Manuari: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jumaa la leo kwa kutupa uhai na uzima, pili nimuunge mkono ndugu yangu Bwana Allen Katana ambae hali kadhalika yeye ni Mwenyekiti wa elimu sasa sisi tunajua kwa nini sisi tulimpa uwenyekiti wa elimu, ni kwa sababu kila anapokaa huwaza kuwawekea jamii akiba ya kesho...

[Applause]

Kwa sababu elimu ndio akiba ya kesho. Mimi nimesimama Mheshimiwa Spika kumuunga ndugu yangu mkono na nimalizie kusema Waswahili husema mdharau bio hubiuka. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Manuari. Yes, Honourable Mariam Baimu please make your contribution.

Hon. Baimu: Shukran sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Kwanza ningependa kuunga mkono na kumshukuru sana Mheshimiwa Allen Katana kwa kuleta hoja hii hapa Bunge kusema ukweli sote hapa wananchi wana matarajio makuu sana haswa huu upande wa kazi watu wapate ajira ama wapate pesa za kuwasaidia kimaisha kwa hivyo kimimi kusema ule ukweli kama Waswahili wanavyosema ukim *empower* mwanamke ama mama mama ume *empower* jamii kwa hivyo tunapo wapatia hawa wamama na haswa hawa vijana wetu zile ujuzi waweze kusoma maanake tuna imani moja sio kila mtu atapata ajira ya kufanya kazi kwa ofisi, wengine itabidi wafundishwe kazi za mikono ili waweze kujisaidia katika maisha yao, kwa hivyo kusema ule ukweli hoja ni ya maana sana na sisi kama wawakilishi wa wadi zetu tuzitilie sana maana katika vichwa vyetu tuweze kupitisha hii hoja ili hii kitu iweze kufanyika. Kwa hivyo shukran sana Mungu awabariki.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Baimu. Yes, Honourable Arwa.

Hon. Ojala: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kunipatia fursa hii na mimi nichangie kwa hii swala ilioletwa na Mheshimiwa Allen Katana. Mheshimiwa Spika, mimi nikisimama hapa nampongeza Mheshimiwa Allen Katana kwa swala hili maana ukiangalia kwa jamii yetu ukweli wa maneno kwamba watu wengi wamekaa tu hawajui na nyuma wala ni nini. Maanake ukipata kama saa hii ukivuka upande ule wa Ferry Likoni utapata watu wamejaa sana pale kwa steji ni kwamba wanapiga mdomo na siasa na mtu akifika jioni hata hajui anaenda kula nini. Mheshimiwa Spika, na leo hii ikiwa hili swala litatiliwa maanani utakuwa umetusaidia sana sisi kama viongozi na jamii kwa jumla. Mimi naomba niende nje ya mada dakika moja Mheshimiwa Spika maana kama sitakuwa sitaki kusema haya hata mimi kwa Mwenyezi Mungu nitakuwa nitahukumiwa. Mheshimiwa Spika nakuletea salamu kutoka kwa ile familia uliosaidia jana wazazi aliniambia nikifika hapa kwa Bunge niweze kusimama na kukufikishia salamu yao ni kwamba wamekushukuru sana maana kwa ukweli umetuonyesha njia nzuri kwamba wewe hubagui wala huchangui, twakutakia kila kheri kwa juhudi hiyo na roho hiyo uendelee. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nasimama kuunga mkono swala hili. Shukran Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Arwa. Yes, Honourable Mwalimu.

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Mimi nimesimama kuunga mkono Mheshimiwa mwenzangu wa Shanzu kwa sababu ya kujali vijana wetu na wamama....

[Applause]

...Kiukweli vijana wetu kwa sababu hawashirikishwi kwa shughuli za kila siku ndio maana wao wamejaa mitaani na maskani na kufanya mambo yasiyokuwa mazuri kwa jamii. Lakini kwa Mswada huu ambao umeletwa na ndugu yangu iwapo utatekelezwa basi vijana wetu watachangamka na kuweza kufanya shughuli mbalimbali za kujikimu ki maisha. Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mbarikiwe nyote Waheshimiwa wenzangu.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Mwalimu. Yes, Honourable Hamisi Mwinyi Mtoto?

Hon. Hamisi Mtoto: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa hii fursa ili niweze kuchangia hoja ilioletwa na Mheshimiwa mwenza Allen Katana. Mheshimiwa Spika hii hoja ilioletwa na Mheshimiwa mwenza imenigusa sana hasa kule kwangu kwa sababu Wadi yangu ndiyo yenye umaskini ambao vijana wengi na mama wengi wamekaa bila ya kazi. Kwa hivyo mimi naunga mkono Mheshimiwa mwenza na hili jambo tulifuatilie ili tuwawezeshe wale vijana wetu na mama wetu kule mtaani. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Hamisi yes Honourable Eliud?

Hon. Kimari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika naweza chukua fursa hii kurudishia Mheshimiwa mwenza 1GB almaarufu 1GB shukran. Nilipoona hoja hii jana Mheshimiwa Spika kuwa tutajadili siku ya leo nilisema lazima nifike hata ingawa nilikuwa na safari lakini nilisema lazima nifike juu hoja hii Mheshimiwa Spika ukiangalia idadi ya vijana katika mitaa yetu kule tunako ishi wasio na ajira ni kubwa na ukiangalia katika kila mwaka humu nchini wale wanao hitimu katika universities ama colleges wana range between elfu kumi tano na elfu thelathini na ukiangalia Mheshimiwa Spika zile kampuni ama kupata kazi kwa kampuni ama kwa serikali ni ngumu kwa hivyo inaishia hawa vijana wengi wanaishilia kurudi kule mtaani bila kazi hawa wengine wao wako na talanta kama tunaweza kukuza hizi talanta hawa vijana hawatakaa kule mtaani kwa sababu ukiangalia kule mtaani ukipita hata mambo na ya security, *insecurity* yenye iko kule mitaani kwetu imesababishwa na na ukosaji wa kazi. Tukichukua hawa vijana Mheshimiwa spika tuwapeleke tukuze zile talanta zao kuna wengine ni mafundi wa mbao, kuna wengine wanaweza kuwa ni fundi wa stima, hawatakuwa pale mtaani kutatokea kwa mfano pale mtaani kuna shida ndogo anaenda kutekeleza na kufanya Mheshimiwa Spika na ukiangalia hapo kitambo kuna *cottage industries* sijui kwa Kiswahili mnasema vipi cottage industry ukiangalia Mheshimiwa Spika katika jamii ya Wakamba na jamii ya wa Kikuyu kuna vile vyondo walikuwa wakishona na ukiangalia vile vyondo siku hizi vinatoka uchina na kama ingewezekana vile vyondo tunakuza wanaweza kushona hakuna vile tungetoka hivi twende kuzichukua kule uchina. Kwa hivyo mimi naunga mkono Mswada wa Allen Katana Mkono.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Eliud. Yes, Honourable Allen Katana you may reply for the Motion?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika mimi sina mengi ya kusema kwa sasa kwa sababu hoja hii nilipo ileta sikujua kuwa itapata wenzangu ambao ni waledi zaidi yangu na kuifafanua kwa ujumla. Lililobaki kwangu Mheshimiwa kwanza ni kumshukuru Mheshimiwa mteule Bwana Hamid kwa kuliunga mkono hili swala, ambaye pia ni Mwenyekiti wa chama tawala katika Bunge letu la Kaunti ya Mombasa na tena nimshukuru kiongozi wa wengi hapa Bungeni pamoja na Waheshimiwa wote akiwemo wa Magogoni, Timbwani, Mtopanga, Junda, Likoni, Frere town na dadangu Pamela Mheshimiwa wa Shika Adabu, Mwakirunge na Mkomani. Mheshimiwa Spika, ni ombi langu kupitia kwa Kamati na Mheshimiwa nilikuwa nimemsahau mtoto wa Mheshimiwa wa Likoni Mheshimiwa Manuari. Mheshimiwa, ni ombi langu kupitia kwa Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa wa Kongowea na kwa kuwa Waheshimiwa nimeona hili swala wamelichangia vizuri ni maana swala hili ni la maana sana. Kwa hivyo ningomba Mheshimiwa Spika liwe litafanyiwa kazi kwa haraka ili tukaweze kuyavuna matunda ya maono haya. Kwa hayo machache ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you again Honourable Allen Katana to reply the Motion. Honourable Members, I now put it that the Motion by Honourable Allen Katana MCA Shanzu Ward on establishment of massive vocational training and up skilling of unemployed youth and women programme be approved by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stand adjourn until Wednesday 15th February, 2023.

The House rose at 11:05a.m